


Wakati gani TAM hufanyika?

TAM hufanyika wakati mradi unapoanza kupangwa. Ni lazima kufanyika kabla mradi haujaanza kutekelezwa.



Jinsi gani utashirikishwa?

Mikutano ya mashauriano ya awali:

- Timu za TAM kwa sasa zinafanya mikutano na taasisi mbalimbali za serikali, jamii za wenyeji na wadau wengine kubadilishana taarifa juu ya mradi na uchunguzi wa TAM.
- Unaweza kuuliza maswali na kutoa maoni wakati wa hii mikutano.
- Maoni yako yote yataandikwa na kuzingatiwa.

Uchunguzi wa wataalamu:

- Timu za TAM zitafika Vijijini kwenu kupata taarifa kutoka kwenu kuhusiana na masuala mbalimbali ya kijamii yanayohusu shughuli zenzi za kujikimu (kilimo, uvuvi, biashara, afya, elimu, urithi wa utamaduni, n.k.).
- Watafanya pia uchunguzi juu ya bayoanuwai (mimea, wanyama), udongo, hali ya hewa, kelele, msongamano wa magari, utalii n.k.

Mikutano ya mashauriano ya mrejesho:

- Mikutano mfululizo itafanyika kwa jamii za wenyeji, taasisi za serikali na taasisi zisizo za serikali mara tu baada ya uchunguzi wa wataalamu na TAM vikikamilika ili kujadili matokeo yake.
- Kwa mara nyingine mtaweza kuuliza maswali na kutoa maoni yatakayozingatiwa kwenye ripoti ya TAM.
- Ripoti hizi zitawasilishwa kwa serikali za Uganda na Tanzania ili kutoa idhini yao. Baada ya kuidhinishwa ndipo mradi utaweza kuendelea. Hatua zote za usimamizi zilizobainishwa ndani ya ripoti ni lazima zitekelezwe.

Nani atafanya TAM?

Uchunguzi huu utafanywa na wataalamu kutoka Uingereza (RSK) na Washirika wake kutoka Uganda (ECO & Partners) na Tanzania (JSB, COWI).